

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA NANE

KIKAO CHA NANE

14 SEPTEMBA, 2017



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA NANE

KIKAO CHA NANE – TAREHE 14 SEPTEMBERA, 2017

I. DUA

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Maelezo ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhusu Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Watalaan wa Afya Shirikishi wa Mwaka 2016 (*The Medical, Dental and Allied Health Professionals Bill, 2016*).

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA NA
MAENDELEO YA JAMII:**

Maoni ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Watalaan wa Afya Shirikishi wa Mwaka 2016 (*The Medical, Dental and Allied Health Professionals Bill, 2016*).

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhusu Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Watalaam wa Afya Shirikishi wa Mwaka 2016 (*The Medical, Dental and Allied Health Professionals Bill, 2016*).

MWENYEKITI WA KAMATI YA SHERIA NDOGO:

Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge.

III. MASWALI:



OFISI YA WAZIRI MKUU:

96. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Baadhi ya Wafanyakazi wamejiunga na Mfuko wa NSSF na hukatwa sehemu ya mishahara yao kwa ajili ya kuwekeza ili iwasaidie baada ya kustaafu:-

- (a) Je, mpaka sasa ni Wafanyakazi wangapi wamejiunga na Mfuko huo;
- (b) Je, ni Wafanyakazi wangapi wamestaafu kazi na kulipwa fedha zao na Mfuko huo;
- (c) Je, ni nani analipwa faida inayopatikana kwa fedha za Mfuko huo kutoka Benki zinakowekwa.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

97. MHESHIMIWA JOEL MWAKA MAKANYANGA (CHILONWA):

Atamuuliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Barabara inayounganisha Vijiji vya Msanga na Kawawa ni muhimu sana kiuchumi kwa Kata ya Msanga na Wilaya ya Chamwino na pia mazao mengi ya uhakika kutoka Kawawa na Vitongoji vyake lakini barabara hiyo ni korofi sana kwa sababu ya Mbuga iliyoko katika Vijiji hivyo viwili, na daraja kubwa lililopo limevunjika kabisa kiasi kwamba halipitiki kabisa wakati wa mvua na wakati wa kiangazi hupitika kwa taabu sana:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha barabara hiyo na kulijenga daraja husika ili kuboresha mawasiliano ya Vijiji hivyo viwili na masuala ya usafirishaji.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

98. MHESHIMIWA SUSAN LIMBWENI KIWANGA (MLIMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Jimbo la Mlimba linakabiliwa na miundombinu mibovu ya barabara na kushindwa kuitika kipindi chote cha Mwaka na hivyo kusababisha adha kubwa kwa Wanawake, Watoto, Wagonjwa na pia Wananchi kwa ujumla wanaosafirisha mazao kufuata wanunuzi na huduma za Serikali kama vile kwa Mkurugenzi wa Halmashauri, Mkuu wa Wilaya, Hospitali ya Wilaya, Mahakama na Polisi Wilayani Ifakara:-

- (a) Je, ni lini barabara ya Ifakara - Mlimba - Madeke - Njombe itajengwa kwa kiwango cha lami kwa kuwa upembuzi wa barabara hiyo ulishafanyika;

(b) Wakati tunasubiri barabara ya lami, Je, Serikali ina mpango gani wa kuitengea fedha za kutosha barabara hiyo ili kuifanya ipitike kwa kipindi chote cha mvua na kiangazi.

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

99. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvubi:- Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Watendaji wa Vyama vya Msingi vya Mazao (AMCOS) wanapatikana kwa njia ya ushindani na wanakuwa na sifa zinazostahili.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

100. MHESHIMIWA ALMAS ATHUMAN MAIGE (TABORA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Mahakama ya Mwanzo katika Kata ya Upuge Wilaya ya Uyui imetelekezwa zaidi ya miaka kumi na kusababisha miundombinu yake kuanza kuharibika:-

- (a) Je, ni kwa nini Mahakama hii imetelekezwa;
- (b) Je, ni kwa nini majengo ya Mahakama hiyo yasitumike na Idara nyingine za Serikali.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**101. MHESHIMIWA MARY PIUS CHATANDA
(KOROGWE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Hospitali za Serikali zimeandaliwa kupata huduma za dawa MSD lakini wakati mwingine baadhi ya dawa zimekuwa hazipatikani MSD na Hospitali haziruhusiwi kununua dawa nje ya MSD:-

Je, Serikali imetua maelekezo gani pale ambapo MSD wamekuwa hawana baadhi ya dawa hizo zinazohitajika kwa Wagonjwa.

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

102. MHESHIMIWA ANNE KILANGO MALECELÀ (KUTEULIWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Watanzania wamehamasika sana na Kilimo cha Tangawizi; na zao la Tangawizi kwa sasa linalimwa sio tu na Wananchi wa Wilaya ya Same bali pia katika Mikoa kama Mbeya, Kigoma na Ruvuma:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kulitafutia zao hili Soko la nje.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

103. MHESHIMIWA TWAHIR AWESU MOHAMED (MKOANI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Tanzania ni nchi yenye amani kubwa katika Nchi za Maziwa Makuu:-

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuimarisha amani katika nchi yetu;

(b) Je, mipaka yetu na nchi zenyenye mizozo na Wakimbizi imeimarishwa kiasi gani kiulinzi.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

104. MHESHIMIWA KABWE ZUBERI RUYAGWA ZITTO (KIGOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Nchi ya DRC inategemea Kigoma kiuchumi kwa kiwango kikubwa hususan katika soko la bidhaa na huduma ya Bandari ya Kigoma na hivyo Wananchi wengi wa Kigoma kutembelea Congo na wale wa Congo hutembelea Kigoma; changamoto kubwa ni gharama za biashara kutokana na VISA kati ya nchi hizo mbili licha ya kwamba nchi hizo zote ni wanachama wa SADC na nchi za SADC hazina VISA kwa raia wake:-

Je, ni kwa nini Serikali ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo haziondoi VISA kwa raia wake ili kudumisha biashara kati ya Wananchi wake kwa lengo la kukuza Kigoma kuwa Kituo cha Biashara cha Maziwa Makuu.

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu).

Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Watalaaam wa Afya Shirikishi wa Mwaka 2016 (*The Medical, Dental and Allied Health Professionals Bill, 2016*).

V. HOJA ZA KAMATI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA SHERIA NDOGO:

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge.

DODOMA
14 SEPTEMBA, 2017

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE